HABARI LEO UK 8.

# Ndaki: Mkandarasi asimamishwe kazi

**Na Mwandishi Wetu, Tanga**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki amemuagiza Katibu Mkuu anayesimamia Sekta ya Mifugo kumsimamisha kazi mkandarasi anayejenga miundombinu ya mnada wa Ndelema wilayani Handeni kwa kushindwa kufanya kazi kwa wakati.

Ndaki alitoa agizo hilo jana baada ya kukagua ujenzi wa miundombinu ya mnada huo ambapo wakati anapita, hakukuwa na kazi inayoendelea na mkandarasi hakuwapo kwenye eneo la ujenzi.

Pamoja na agizo hilo la kusitisha mkataba wa mkandarasi huyo, Ndaki pia ameagiza kusitishwa kwa malipo ambayo yalikuwa yapo kwenye mchakato kwa kuwa mkandarasi huyo hastahili kulipwa kutokana na kazi aliyoifanya.

Aidha, alimuagiza Katibu Mkuu anayesimamia Sekta ya Mifugo kumtafuta mkandarasi mwingine mwenye uwezo wa kufanya kazi hiyo kwa wakati ndani ya siku 14 iweze kuendelea.

"Serikali ilishatenga fedha za kutosha kwa ajili ya kuhakikisha miundombinu ya mnada inajengwa ili kuwawezesha wafugaji kuuza mifugo yao katika mazingira mazuri na kusaidia katika kuongeza ukusanyaji wa maduhuli, hivyo haitamvumilia mkandarasi yeyote mzembe," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Siriel Mchembe alisema mnada huo ni muhimu katika ukusanyaji wa maduhuli ya halmashauri.

Alisema ucheleweshwaji wa ujenzi wa miundombinu yake unakwamisha maendeleo ya Mji wa Handeni kwani mapato yangepatikana kupitia fedha ambazo zingekusanywa hapo.

Mkurugenzi wa Idara ya Huduma za Mifugo, Profesa Hezron Nonga, alisema mkandarasi huyo alishaandikiwa barua ya onyo kutokana na ucheleweshaji wa ujenzi wa mnada huo mbali na kuitwa wizarani kwa lengo la kumtaka akamilishe kazi aliyopewa ya ujenzi wa miundombinu kwenye mnada wa Ndelema.

Scanned with CamScanner

THE GUARDIAN Page 13

# Zones livestock sale registered 460bn/-revenue in Q4 of 2021

By Guardian Reporter



A customer holds a goat before buying it at one of the livestock markets in Dar es Salaam. PHOTO/FILE

LIVESTOCK sales in Tanzania mainland official markets registered a slight increase of revenue by 2bn/- to 460bn/- during the fourth quarter of last year from 458b/- recorded during similar quarter of 2020, Bank of Tanzania (BOT) has reported.

According to the consolidated zonal economic report for Q4, 2021 published late last week, total value of livestock sold during the third quarter of last year amounted 610bn/-.

Data by Regional Secretary Offices and BOT say an increase was largely driven by price was observed in Lake Zone ad Southern Highlands Zone, while the remaining zones recorded a decrease in reveune.

Lake Zone, which accounts for 26.7 percent of total livestock trade in Tanzania mainland, a total revenue amounting 122bn/- was recorded during the fourth quarter of last year from 106bn/- recorded during Q4, 2020.

The second largest market is Central Zone where the amount slightly decreased to 102bn/- from 117bn/- or 22.3 percent of total market value, followed by Northern Zone, where the value of livestock sold amounted 117bn/- from 113bn/- respectively.

According to the report, the Southern Highlands, which accounts for 5.3 percent of total market share, recorded livestock sale amounting 24.4bn/- from 22.6bn/- respectively, while the eastern southern zone, which accounts for 5.2 percent of total markets share sold livestock valued 26bn/- during Q4, 2021 from 24bn/- in Q4, 2020.

Cattle trade remained dominant accounting for 89.5 percent of the total value of livestock sold in the markets, according to the report.

The value of cattle sold during the period reviewed increased to 412.1bn/- in the fourth quarter of last year, of which Lake Zone sold 111.5bn/-, Central zone had 93bn/- and Northern zone with 100bn/- while in Q4, 2020 a total value amounted 408bn/-.

The value of cattle sold in Dar es Salaam zone slowed to 61.6bn/- in 2021 from 67.7bn/ recorded during similar quarter of 2020 due to decrease in price, although number of cattle sold increased to 64,824 from 62,525 respectively.

The report shows that the value of goats sold in all markets increased to 38.7bn/ during the third fourth last year from 40.6bn/- in Q4, 2020, but number of goat sold slightly increased to 451,116 from 436,951 respectively.

Northern zone had the largest value of goat sold amounted 13.5bn/- out of total revenue amounting 38.7bn/- followed by Lake Zone with 8.5bn/-.

The value of sheep sold during the last quarter of last year was 9.5bn/- of which Northern Zone had the largest share with 3.9bn/- followed by Lake zone with 2.7bn/-.

Scanned with CamScanner

# Wafugaji sita matatani wakidaiwa kuharibu mazao

Na Sifa Lubasi

WAFUGAJI sita wanashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa kuingiza ng'ombe mashambani, kuharibu na kufyeka zaidi ya ekari 500 za mahindi na alizeti katika Kijiji cha Izava Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka juzi alifanya ziara kukagua mashamba yaliyoharibiwa na wafugaji katika Kitongoji cha Wali Kijiji cha Izava.

"Kama umeamua kufuga jiheshimu, kuanzia sasa mtu akilisha mifugo shambani kwa mkulima atalipa mahindi magunia 15 kwa kila ekari itakayoharibiwa na alizeti magunia 12, kachunge shambani kwako, sitaleti ninawaambia, DC (mkuu wa wilaya) alifanya mkutano, mkapeleka ng'ombe mashambani, leo na mimi nipo hapa pelekeni," alisema.

Mmoja wa wakulima, Omar Issa alisema shamba lake la ekari 80 limeharibiwa ikiwamo ekari 50 za alizeti na ekari 30 za mahindi. "Hii alizeti nilipanda kwa kutumia mashine ya kupandia, mbegu niliyotumia ya Sh milioni 15," alisema.

Alisema ameingia mkataba na kiwanda cha kuzalisha mafuta ya alizeti cha Pyxus Agriculture Tanzania ambao wamemkopesha mbegu ili akuvune awauzie alizeti.

"Hili shamba limefyekwa lote siwezi kuvuna kitu hapa naomba serikali itusaidie tupate haki yetu, tulihamasishwa kulima alizeti lakini hali ndio kama hii unayoiona, alizeti yote imefyekwa na mahindi yote pia," alisema.

Mkulima mwingine Ryoba Chacha alisema kuwa alikodi shamba kwa ajili ya kilimo cha alizeti na kulima ekari 85 na kutumia Sh milioni nane lakini lote limeharibiwa na ng'ombe.

Mwenyekiti wa wakulima kitongoji cha Wali, Martin Ulaya alisema walianza kupata mashambulizi kutoka kwa wafugaji kuanzia Februari mwaka huu, baada ya malalamiko yao kufika ngazi ya wilaya.

Alisema Mkuu wa Wilaya ya Chamwino, Gift Msuya alifika kijijini hapo, Aprili mwaka huu na kufanya mkutano wa hadhara na alipoondoka, wafugaji walienda kuswaga ng'ombe na kuingiza mashambani.

Kwa mujibu wa Msuya, mpaka sasa ekari zilizofyekwa ni 526 na wakulima 76 wameathirika na uharibifu huo.

Mkazi wa Izava, Robert Mkosa alisema chanzo cha mgogoro huo ni mpaka unaotenganisha Chamwino na Kongwa ambao unapita katikati mbuga. Alisema mgogoro huo ulianza mwaka 2010 baada kijiji jirani kikisema ni eneo la malisho.

Mkuu wa Mkoa alisema timu ya upimaji itapita kuhakiki mpaka kati ya Chamwino na Kongwa. Alisema kuwa lazima kuwe na adhabu itakayolipa mashamba yaliyoharibiwa.

"Suala hili litapiriwa na kuingizwa Kituo cha Polisi ili kulinda wanaolishaji, hapa kuna uzalishaji mkubwa, ni vyema kila mkulima akatambuliwa," alisema.

Akizungumza na wafugaji katika Kijiji cha Ngutoto Wilaya ya Kongwa, Mtaka alisema lazima wafugaji waliohariibu mazao walipe gharama.

Kiongozi wa mila wa Kimasai, Leiba Lemalele alisema ugomvi wa mbuga ni wa muda mrefu ukihusisha mpaka kati ya Chamwino na Kongwa. Alisema kuna wakati ng'ombe 74 wa wafugaji walipotea.

Awali Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Remidius Emmanuel alisema alifanya mikutano kadhaa na wafugaji na upimaji wa eneo hilo utaleta mwafaka.



Scanned with CamScanner